# Urudiaji wa Kisimulizi na wa Kisemantiki kama Mtindo katika Tenzi: Utenzi wa *Seyidina Ali na Mudhari Bin Darimi*

*Aloo Ronald Odhiambo* na *Kineene wa Mutiso*
*Chuo Kikuu cha Nairobi*

**Ikisiri**

**Riwaya na tamthilia kama tanzu za fasihi ya Kiswahili ni mazao ya karne ya ishirini, tofauti na utenzi ambao uliandikwa mara ya kwanza katika mwaka wa 1570. Sifa moja kuu tena ya kimsingi katika utanzu wa ushairi hasa utenzi ni matumizi ya urudiaji wa kisimulizi na ule wa kisemantiki. Sifa ya urudiaji wa kisimulizi na wa kisemantiki ambayo ni wazi kabisa katika maisha ya binadamu ina utata wake unaotokea katika vipengele mbalimbali. Urudiaji wa kisimulizi na wa kisemantiki hutokea katika viwango mbalimbali na vipengele hivyo ndivyo kiini cha fani na maudhui. Licha ya kazi na umuhimu wa urudiaji wa kisimulizi na wa kisemantiki katika tenzi za Kiswahili, kwa uelewa wetu hakuna uhakiki wa kina ambao umefanywa katika vipengele hivi, licha ya utenzi kuchunguzwa sana. Yaliyomo ni mambo ya kijumla kuhusu urudiaji wa kisimulizi na wa kisemantiki ambayo hayajaangazia majukumu na umuhimu huo. Kazi nyingi zimekosa kuhakiki kwa kina urudiaji wa kisimulizi na wa kisemantiki kama mtindo katika ushairi. Kwa hivyo, katika makala haya, lengo letu limekuwa kujadili kwa kina urudiaji wa kisimulizi na wa kisemantiki kama mtindo unaofanikisha fani na maudhui katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*.**

**Maneno Muhimu**: *Utenzi, Umitindo, Uchimuzi, Urudiaji wa Kisimulizi, Urudiaji wa Kisemantiki, Urudiaji wa Kiesajesia, Urudiaji wa Semiki*

**Utangulizi**

Urudiaji ni mbinu inayotumiwa na mtunzi kama njia ya kuzua hisia mbalimbali kwa msomaji. Naye Wales (2001:341) anaelezea kuwa mtunzi wa utenzi hutumia urudiaji kuonyesha kuwa msomaji hajaamini suala linalozungumziwa katika matini. Isitoshe, urudiaji hutumiwa ili kuonyesha imani fulani, hisia za kukwaza, mshtuko na pia kama njia ya kuonyesha mambo ya kiajabu. Vifungu vya maneno mara nyingi vinarudiwa kama njia ya kufanikisha mawazo yasiyoelezeka kwa njia ya moja kwa moja.

Kwa upande mwingine urudiaji wa kisimulizi ni urudiaji unaohusu kutokea tena kwa hadithi inayokumbukwa na kusimuliwa tena katika masimulizi mengine kwa undani wake wa dhana. Aristotle (1967) anasema kuwa hadithi hiyo inayosimuliwa tena lazima iwe na sehemu tatu za kawaida. Sehemu ya mwanzo, kati na mwisho. Kwa mujibu wa Polkinghorn (1995:5), matukio ambayo hutendeka katika hadithi huingiliana kwa mipangilio maalum kwa kutumia misuko. Naye Wamitila (2008:495) anaeleza kuwa urudiaji wa kisimulizi una nafasi muhimu katika kusoma na kuelewa utenzi, mathalani *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*. Kwa maoni yetu, urudiaji huu wa kisimulizi ndio chanzo cha burudani kwa msomaji anaposoma utenzi.

Urudiaji wa kisemantiki kwa upande mwingine unahusu kutokea kwa maana maalum mara nyingi au zaidi ya mara moja bila kurudiwa kwa uelementi wa neno au maneno hayo kwa njia rasmi. Ikumbukwe kuwa lugha ya binadamu kama mchakato mzima, hujaa kuzoelewa kwa maana kutoka kwa umbo la neno lenye mpangilio na kubakisha umbo hilo kwa muda mfupi. Kwa mujibu wa Tsur (2008), urudiaji wa kisemantiki ni mbinu mojawapo ambayo inatumiwa na mtunzi ili kupunguza kasi ya kuelewa ujumbe wa utungo na kuzua athari ya kishairi.

Vivyo hivyo, mtunzi wa *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* hajaachwa nyuma katika kutumia urudiaji wa kisimulizi na wa kisemantiki katika kuleta athari maalum katika utungo huu.

Kwa hivyo, tunachunguza urudiaji wa kisimulizi na wa kisemantiki kama mbinu ya kimtindo inayofanikisha fani na maudhui katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*.

**Mhutasari wa Utenzi**

*Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* ni miongoni mwa utenzi kongwe ambao mtunzi wake hajulikani. Hata hivyo, utenzi huu wenye beti 776 (mia saba sabini na sita) ulihaririwa na J. Knappert mnamo 1964. Katika utenzi huu, mtunzi anazungumzia masuala mbalimbali yanayohusu dini ya Kiislamu. Masuala haya yanawasilishwa na Mudhari bin Darimi na Sheikh Ali. Mambo yanayoibuka katika utungo huu ni pamoja na suala la uumbaji. Mtunzi anasema kuwa Mungu aliumba vitu vingi ila vinne pekee ndivyo vitakatifu. Vitu hivi ni kama vile Malaika, Mitume, milima, masiku, miezi na wanawake. Vilevile nambari nne imetumiwa na mtunzi ili kuonyesha utakatifu, utukufu na ukamilifu katika dini ya Kiislamu. Nambari hii imetumiwa kama nambari ambayo haina dosari katika dini ya Kiislamu.

Mtunzi amezungumzia hadithi ya Ali bin Talib anayejibu maswali ishirini ambayo anaulizwa na mgeni Mudhari bin Darimi anayewasili kutoka Mecca pindi tu baada ya kifo cha Mtume Muhammad kama njia ya kuzuia maswali mengi kutoka kwa Sheikh Ali. Isitoshe maswali haya yanatumiwa kuimarisha imani yake katika dini. Sheikh Ali anathibitisha kuwa anayafahamu maswali haya kwa kutoa majibu sahihi. Maswali haya kwa kiwango kikubwa yametolewa katika Bibilia. Usimulizi wa Sheikhe Ali kuhusu kisa na Musa na Mariamu ndio unaosisimua zaidi. Hatima ya Mwislamu Siku ya Kiyama itajikita katika maswali haya. Isitoshe, maswali haya ndiyo nguzo, msingi na mhimili wa dini ya Kiislamu na maisha ambayo Mwislamu anatarajiwa kuishi akiwa hapa duniani.

Pamoja na hayo, kupitia kwa kisa cha maubiri ya Abu Bakari kuhusu majukumu mbalimbali katika dini ya Kiislamu, mtunzi ametoa wosia kwa Mwislamu kuhusu adhabu atakayopata Siku ya Kiyama iwapo hataweza kuishi kulingana na sheria za dini ya Kiislamu. Mwislamu anatahadharishwa kuwa atapata adhabu kali kule Jehanamu iwapo hatafuata dini. Kwa upande mwingine, Waislamu waliofuata dini wameahidiwa maisha mazuri ya Peponi. Isitoshe, wanakumbushwa kuwa dunia hii siyo makao yao kwa vile wao ni wapita njia tu. Kwa hivyo, ni vyema wajihadhari na anasa ya dunia. Katika utafiti huu, tunajikita katika kuhakiki jinsi mtunzi ametumia urudiaji wa kisimulizi na wa kisemantiki ili kufanikisha fani na dhamira mbalimbali katika utenzi huu wa *Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*.

**Msingi wa Kinadharia**

Utafiti huu unaongozwa na nadharia ya Umitindo ambayo mawazo yake yalitumiwa kwa mara ya kwanza na Leech (1969:2) katika ushairi. Katika kazi yake, anaelezea kuwa nadharia hii inaweza kutumiwa kuhakiki na kutoa fasiri katika kazi za kiisimu na zile za kifasihi. Sababu yake ni kwamba vipengele vya kifasihi haviwezi kujisimamia vinapohakikiwa. Kwa maoni yetu mtindo unarejelea matumizi ya lugha kimuktadha katika kuwasilisha ujumbe. Kipengele cha Umitindo ambacho tunashughulikia katika makala haya ni uchimuzi na mtindo kwa sababu ni vigumu sana kuvishughulikia vipengele vyote vya Umitindo kwa undani kama anavyodai Wamitila (2008:511). Aidha, Wamitila anasisitiza kuwa ni vigumu kueleza vipengele mbalimbali vya kifasihi kama vile urudiaji wa kisimulizi na wa kisemantiki bila kuvihusisha vipengele hivi na vile vya kiisimu.

Tunasema kuwa urudiaji ni mbinu ya uchimuzi wa kimtindo ambao hutokea wakati mtunzi anakiusha lugha katika kazi yake kwa madhumuni ya kuweka wazi jambo ambalo analizungumzia. Uchimuzi unatokea katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* wakati mtunzi anatumia urudiaji na mbinu mbalimbali za urudiaji huo ambao ni sifa za kibalagha za utenzi. Urudiaji na mbinu za urudiaji huo unatokea katika kiwango cha usimulizi na semantiki (maana). Maelezo haya yanatusaidia katika kuchunguza urudiaji wa kisimulizi na wa kisemantiki kama mtindo unaotumiwa na mtunzi katika kuwasilisha fani na maudhui katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*.

Leech (1969:2) anaeleza kuwa kipengele cha uchimuzi na mtindo kinasaidia katika kubainisha sheria ambazo zinatumiwa na mtunzi kuteua maneno maalum katika lugha kama vile urudiaji wa

kisimulizi na wa kisemantiki ili kutekeleza jukumu la uwasilishaji na upokeaji wa maana ya ujumbe, uhakiki wa diskosi na fasihi. Aidha, uchimuzi na mtindo husaidia katika kuchunguza vipengele hivyo vya kifasihi kisayansi kwa kufuata utaratibu wa kitaaluma. Kwani uchimuzi na mtindo huchunguza kile kinachosemwa na jinsi jambo linavyosemwa. Hili linatusaidia katika kuchunguza jinsi mbinu ya urudiaji wa kisimulizi na wa kisemantiki inatumika katika kuwasilisha fani na maudhui katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*.

Mhimili wa Umitindo ambao unatuongoza katika utafiti wetu ni; uhakiki wa kimtindo ni wa kifasihi na kiisimu. Vipengele hivi viwili vinakamilishana kwa vile urudiaji wa kisimulizi na ule wa kisemantiki hauwezi kusijisimamia kivyao ili kujieleza. Mhimili huu unauhusishwa na ujumbe na jinsi ujumbe huo unatolewa kupitia kwa matumizi ya mbinu ya urudiaji wa kisimulizi na wa kisemantiki. Mhimili huu unatusaidia katika kubainisha aina mbalimbali za urudiaji wa kisimulizi na wa kisemantiki na vile mbinu hizi zinatumiwa kuwasilisha ujumbe na kufanikisha fani na maudhui katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*.

**Uchanganuzi**

Mtunzi wa *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* anaangazia masuala anuai yanayohusiana na dini ya Kiislamu. Tumeainisha namna mtunzi anaangazia aina tofauti tofauti za urudiaji wa kisimulizi na wa kisemantiki. Tumeonyesha vile mbinu hizi za kimtindo zinavyofanikisha vipengele mbalimbali vya fani na dhamira. Isitoshe, vipengele hivi ndivyo msingi wa ujumbe unaowasilishwa kuhusu Siku ya Kiyama na maisha ya sasa na yale ya baadaye katika dini ya Kiislamu. Ujumbe kuhusu toba ni kama chanzo cha maisha mema ya Peponi. Kwa upande mwingine ukiukaji wake unaleta maangamio makubwa kule Jehanamu.

**Urudiaji wa Kisimulizi**

Tunaeleza kuwa urudiaji wa kisimulizi hutokea taarifa fulani ya kisimulizi inaposimuliwa tena kwa kina chake. Urudiaji wa kisimulizi unategemea jambo ambalo msomaji au msikilizaji anataka kujua kwa ajili ya kupata uelewa wa zaidi juu ya hadithi. Msimulizi huchanganya usimulizi wake na maana ambayo anakusudia kueleza huku akizingatia hali halisi ambayo inaakisi kile ambacho anayesimulia amewahi kupitia. Kwa mfano, hadithi ya Siku ya Kiyama imerudiwa huku mtunzi akizingatia hali halisi ya waja kuteseka Jehanamu wakipitia mateso mbalimbali kama vile; kuumwa na majoka, kuchomeka kwa moto isiyoisha na hata kukaa njaa bila chakula. Waja walio motoni wanaonyeshwa wakiwa na miili iliyodhoofika sana. Isitoshe, kisa hiki cha Siku ya Kiyama kinafika kilele chake mtunzi anapotuonyesha hali ya furaha kwa waja waliofuata sheria za dini ya Kiislamu wanaposherehekea Peponi. Aidha, waja hawa wana miili iliyonawiri sana.

Wakati mwingine urudiaji wa kisimulizi hutofautiana katika kiwango cha wahusika kwa vile vipengele vinavyorudiwa huchaguliwa. Hata kama taarifa ya kisimulizi inayorudiwa imekuwa zaidi kuliko ile ya awali, wazo kuu katika taarifa ya kisimulizi ya kwanza huwa halibadiliki kwani linabakia kuwa vilevile (Whelan, Huber, Rose, Davies na Clandinin 2010). Hivyo basi, katika sehemu hii tunaangazia aina mbalimbali za urudiaji wa kisimulizi kama unavyotokea katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*.

**Urudiaji wa Vitushi**

Urudiaji katika kiwango cha vitushi ni aina ya urudiaji wa kisimulizi inayohusu kusimuliwa kwa kisa tena na tena katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* huku kina chake kikizingatiwa. Mtunzi wa utungo huu amerudia hadithi mbalimbali katika beti tofauti tofauti. Hadithi hizi ni pamoja na; hadithi ya dini ambayo imesimuliwa katika beti za mwanzo na pia katika beti za mwisho (ubeti wa 1- 32 na 772- 776). Katika hadithi hii, mtunzi anaanza usimulizi wake kwa sala maalum kisha anawasimulia Waislamu kwa kuwatahadharisha ya kwamba wajiepushe na maovu kwani maovu yatawaelekeza katika hukumu Jehanamu. Aidha, hadithi hii inasimuliwa tena katika beti za mwisho (772 - 776) mtunzi anapowaombea dua Mtume Muhammad pamoja na familia yake. Isitoshe kitushi hiki cha kidini kimesheheni katika utungo wote. Urudiaji wa hadithi hii, unaleta dhamira ya toba na wahusika mbalimbali kama vile Allah, Mtume Muhammadi, malaika na Waislamu ambao

wamesheheni katika visa na vitushi mbalimbali katika utungo huu na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kukuza urudiaji wa kisimulizi.

Pili, kitushi kuhusu Siku ya Kiyama vilevile kimesimuliwa katika ubeti wa 21 na kurudiwa katika beti za 640 – 653 na 690 - 691. Hadithi hii ni msingi wa utenzi huu. Kwa vile inaongoza matukio mbalimbali yanayotendwa na Waislamu katika utungo. Isitoshe, maisha ya Mwislamu yanaongozwa na matukio yatakayojiri siku hii ya mwisho. Urudiaji wa kitushi hiki kinachangia katika ukuaji wa vipengele mbalimbali vya fani na dhamira katika utenzi huu na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kukuza urudiaji wa kisimulizi.

Kitushi kingine kinachorudiwa ni hadithi ya uumbaji katika ubeti wa 33 hadi 63. Katika hadithi hii, mtunzi anaelezea uwepo wa vitu tofauti tofauti duniani, uwepo wa wanyama, malaika, siku, wanadamu na hata mlima. Katika kitushi hiki, mtunzi anazungumzia uumbaji wa vitu katika unne. Usimulizi wa hadithi ya uumbaji unaleta dhamira ya uumbaji na chanzo cha uwepo wa wahusika mbalimbali. Dhamira hii imekuzwa katika vitushi mbalimbali katika utungo huu na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kukuza urudiaji wa kisimulizi. Kwa upande mwingine, kuna hadithi ya kifo cha Mtume Muhammad na sifa zake zinazorudiwa katika ubeti wa 64 – 175. Aidha, hadithi ya Nuhu pia inarudiwa katika ubeti wa 201 hadi 208. Hadithi hii ni kati ya hadithi inayotukumbusha kuhusu mambo yaliyotukia zamani wakati waja walipokataa kufuata kanuni za Mungu. Mtunzi ameonyesha matumizi ya mbinu rejeshi katika usimulizi wa hadithi hii. Usimulizi wa vipengele mbalimbali tena na tena katika vitushi hivi unachangia katika kujenga urudiaji na kwa jinsi hii kukuza urudiaji wa kisimulizi.

Vilevile hadithi ya Ibilisi pia imesimuliwa katika ubeti wa 557 hadi 580. Hadithi hii inaleta mbinu ya kinaya katika utungo huu mtunzi anaposimulia kuhusu vitu vinavyopendwa na Ibilisi na vile anavyovichukia. Mbinu ya kinaya inatumika wakati Ibilisi anaposema kuwa anavichukia vitu vyote vinavyopendwa na Mungu huku akivipenda vile vinavyochukiwa na Mungu. Aidha, anasisitiza kuwa anawapenda sana watu waovu. Kuna urudiaji wa hadithi kuhusu mambo manne muhimu kwa Mwislamu (ubeti wa 594 hadi 628). Usimulizi huu unachangia katika kujenga urudiaji vipengele vya vitushi hivi vinaposimuliwa tena na tena na kwa jinsi hii kuendeleza urudiaji wa kisimulizi.

Pamoja na hayo, kuna hadithi ya Abubakari katika ubeti wa 673 – 692. Katika hadithi hii, Abubakari anatoa mahubiri kuhusu majukumu katika dini ya Kiislamu. Mtunzi anayasisitiza mambo yatakayompata Mwislamu mwishowe dunia itakapofika mwisho. Hadithi hizi kwa ujumla, zimechangia ukuaji wa wahusika mbalimbali pamoja na sifa zao. Wahusika hawa ni pamoja na; Mungu, ibilisi, Mtume Muhammadi, Malaika, Shekhe Ali na Mudhari bin Darimi. Kupitia kwa matendo na sifa za wahusika, mtunzi anaendeleza msuko wa utungo huu. Vilevile wahusika hawa pamoja na sifa zao zimesheheni katika vitushi mbalimbali na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kukuza urudiaji wa kisimulizi.

**Urudiaji wa Wahusika na Matendo yao**

Katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*, wahusika mbalimbali pamoja na matendo yao yamerudiwa kwa ustadi mkubwa kama njia ya kukuza dhamira na msuko wa utungo huu. Kwa mfano, wahusika kama vile Allah, Waislamu, Malaika, Ibilisi, Mtume Muhammadi na Isa wamerudiwa katika beti tofauti tofauti katika kazi hii. Kupitia kwa urudiaji wa wahusika hawa pamoja na matendo yao, mtunzi ameweza kukuza dhamira kama vile; toba, uovu, hukumu, uokovu na wema. Urudiaji wa dhamira hizi zinachangia katika kujenga urudiaji na kwa jinsi hii kukuza urudiaji wa kisimulizi.

Mhusika kama vile Mtume Muhammad anawahimiza wafuasi wa dini ya Kiislamu kutenda mema siku zote kama njia ya kipekee ya kuenda Peponi. Isitoshe, mhusika Ibilisi anawasisitizia Waislamu kuwa ni vyema kutenda maovu kama njia ya kufurahia maisha ya duniani na kujiepusha na mambo ya Mungu. Kupitia kwa matendo ya wahusika hawa, sifa tofauti tofauti za wahusika mbalimbali zinakuzwa. Isitoshe, mazingira ya Jehanamu na Peponi vilevile yanakuzwa kwa vile matendo mema yatawaelekeza Waislamu Peponi huku yale maovu yanayopendwa na Ibilisi yakiwaelekeza Jehanamu.

Urudiaji huu wa wahusika unachangia katika kujenga urudiaji na kwa jinsi hii kukuza urudiaji wa kisimulizi.

**Urudiaji wa Matukio**

Urudiaji wa tukio ni aina ya urudiaji wa kisimulizi inayotokea tukio moja linaposimuliwa tena katika vitushi vingine au kama tukio jipya ama wakati tukio lililotokea hapo awali likitukia katika akili ya mhusika fulani. Aidha, urudiaji wa tukio linaweza kutokea wakati tukio lililofanyika katika akili ya mhusika likitokea kwa mara ya pili katika utungo au tukio hili likifanyikia wahusika wengi ama tukio hilo linaposimuliwa na mtunzi.

Katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*, tukio la hukumu Siku ya Kiyama limesimuliwa kwa mara ya kwanza na mtunzi katika ubeti wa 21. Tukio hili linahusu namna ambavyo watu watahukumiwa kwa kutegemea kiwango chao cha dhambi siku ya mwisho. Tukio hili limerudiwa katika ubeti wa 135B hadi 135C, 140- 148, 640-643 na 690 mpaka 698. Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa ni tukio ambalo limesheheni katika utenzi wote. Sababu yake ni kwamba tukio hili limerudiwa katika vitushi mbalimbali katika utungo huu. Tukio hili linachangia katika kuleta aidha maisha mazuri ya Peponi ama maisha ya kuteseka kule Jehanamu.

Kupitia kwa urudiaji wa tukio hili na mtunzi, tunasisitiziwa kuhusu maisha mema yanayostahili kuzingatiwa na Waislamu. Kwani mtunzi anasimulia maisha mazuri ya baadaye ambayo Mwislamu anayezingatia mafundisho ya dini ataishi huku yule aliyepuuza dini akitesekea moto ya Jehanamu yenye majoka yanayouma. Urudiaji wa tukio hili linachangika katika ujenzi wa urudiaji na kwa jinsi hii kukuza urudiaji wa kisimulizi.

Isitoshe, kuna tukio la kabila kumuua nduguye Habila baada ya Mungu kumkataza kumuoa kwa lazima. Tukio hili limerudiwa katika utungo huu. Kupitia kwa tukio hili, mtunzi anaendeleza dhamira ya mauaji inayoendelezwa katika vitushi mbalimbali na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kukuza urudiaji wa kisimulizi. Zaidi ya hayo kuna tukio la uumbaji linalotokea kwa wingi katika utenzi huu. Katika tukio hili, mtunzi anaelezea tukio la Mungu kuumba vitu vingi duniani ila vinne tu ndivyo vitakatifu. Tukio hili ndilo chanzo cha kuendelea kwa matukio mbalimbali katika utenzi huu na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kukuza urudiaji wa kisimulizi.

Tukio lingine lililosheheni katika utungo huu ni tukio la kuomba. Katika tukio hili, Waislamu wanahimizwa kuomba kila wakati kama njia ya kipekee ya kujiepusha na majanga yatakayowazuia kuenda Peponi Siku ya Kiyama. Tukio hili na kati ya matukio viini katika utungo huu kwa kuwa ni msingi wa matendo mbalimbali na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kukuza urudiaji wa kisimulizi. Kwa ujumla mtunzi anapotumia urudiaji wa matukio katika utungo huu, basi anakuza mazingira mazuri ya Peponi na mazingira ya kuogofya ya Jehanamu. Isitoshe, usimulizi huu unachangia katika kuleta dhamira ya toba na hukumu. Shughuli na matendo mbalimbali ya wahusika pia yanakuzwa kupitia kwa urudiaji huu wa matukio na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kukuza urudiaji wa kisimulizi.

**Urudiaji wa Kisemantiki**

Kwa maoni yetu, urudiaji wa kisemantiki unatokea wakati maana fulani inaporudiwa katika utungo zaidi ya mara moja huku mtunzi akitumia maneno mengine tofauti na yale ya awali. Mtunzi hutumia njia mbalimbali za lugha katika utungo ili kuwasilisha maana. Njia hizi zinaweza kuwa pamoja na; kukaribiana kwa maneno, nafasi ya kisintaksia na msisitizo. Aidha, njia hizi zimebeba habari zaidi kwa mfano, wakati mtunzi anarudia maneno yale yale ambayo ni muhimu sana kwa msomaji.

Matukio hurudiwa katika urudiaji wa kisemantiki kama sehemu ya mipangilio wala si kibahati. Stanhope, Cohen na Conway (1993) wanatoa kauli kuwa, elementi za kisemantiki zinazorudiwa hukumbukwa kwa kipindi kirefu zaidi bila kusahaulika ikilinganishwa na elementi za kawaida. Haya hutokea kwa sababu urudiaji wa kisemantiki unadumu kwa muda mrefu huku ule wa kawaida ukififia baada ya muda mfupi.

Urudiaji wa kisemantiki unatokea kwa vipengele vidogo kama vile matukio hadi kwa vipengele vikubwa ambavyo vinapanuliwa kutoka kwa maandishi tofauti tofauti. Kwa mfano, mhusika

Abubakari anapokumbuka jinsi Mungu alivyoharibu dunia kule Sodoma na Gomora katika maubiri yake kuhusu mafunzo muhimu katika dini ya Kiislamu katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*. Isitoshe urudiaji wa kisematiki unaweza kutokea wakati tukio moja linapokuwa na mwonoulimwengu sawa kwa wahusika wawili tofauti. Zaidi ya hayo, urudiaji huu hutokea wakati matukio mawili katika utungo yanaporejelea kitu kimoja. Katika uchunguzi wetu, tunahakiki urudiaji huu kwa undani zaidi kama njia ya kuelewa jinsi urudiaji wa kisemantiki unavyofanikisha fani na maudhui katika utenzi huu wa *Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*. Mtunzi wa utungo huu ametumia aina mbambali za urudiaji wa kisemantiki. Aina hizi ni pamoja na:

**Urudiaji wa Semiki**

Urudiaji wa semiki ni urudiaji changamano unaotokea wakati neno linalorudiwa linaweza kugawanywa katika makundi madogo yenye sifa bainifu. Isitoshe, sifa hizi ni tofauti na nyingine. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*, maneno **Peponi** na **Jehanamu** ambayo yamerudiwa sana yana sifa bainifu. Sifa hizi ni kama zifuatazo;

**Peponi**: +sifo, +furaha, +mwangaza, +utulivu, +kunawiri, -kudhoofika, -kulia, -kelele.

**Jehanamu**: +maangamio, -sifo, - furaha, +giza, -utulivu, -kunawiri, +kudhoofika, +kulia, +kelele.

Urudiaji huu wa semiki unaonyesha sifa bainifu za mazingira ya Peponi na Jehanamu na unachangia katika kutuonyesha hali itakavyokuwa Siku ya Kiyama. Urudiaji huu unachangia katika kuendeleza dhamira ya toba na hukumu siku ya mwisho ambayo ndiyo masuala ya kimsingi yanayozungumziwa na mtunzi wa utenzi huu. Isiitoshe masuala haya yamesheheni katika utungo huu na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kukuza urudiaji wa kisemantiki.

Vilevile maneno kama vile **Mtume Muhammad** na **Ibilisi** pia yamerudiwa kwa wingi. Maneno haya yanaweza kuleta maana haya kutokana na sifa zao bainifu.

**Mtume Muhammad**: +mkarimu, +mkweli, +mtetezi, +nuru, +uzima.

**Ibilisi**: -ukarimu, +muongo, -mkweli, +giza, -nuru, -uzima, +maangamio.

Mifano hii imetumiwa kuendeleza sifa mbalimbali za wahusika tofauti tofauti wanaopatikana katika utungo huu. Isitoshe, mbinu hii pia imetumiwa ili kuonyesha mkinzano uliopo kati ya wahusika mbalimbali wanaojengwa na mtunzi. Zaidi ya hayo, ni kupitia kwa sifa za wahusika hawa ambapo mtunzi amefaulu katika kuendeleza dhamira ya toba iliyosheheni katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kukuza urudiaji wa kisemantiki.

**Urudiaji wa Kisawe**

Urudiaji wa kisawe au sinonimia ni urudiaji ambao mara nyingi unatumiwa na mtunzi kukuza wazo wakati anatumia neno lingine lenye maana sawa na lile la kwanza alilotumia. Urudiaji huu umetokea katika *Utenzi wa seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*. Kwa mfano, katika ubeti wa 292 kuna neno **simba wa Mungu,** neno hili pia limetumika katika ubeti wa 536 mtunzi anapotumia neno **simba wa Mannani**. Neno Mannani ni kisawe cha Mungu. Neno hili limetumiwa na mtunzi kama njia ya kuzuia uziada. Vilevile ni neno linaloonyesha kuwa Sheikhe Ali ni mtetezi wa Mungu na dini ya Kiislamu kwa ujumla.

Pamoja na hayo, katika ubeti wa 65 neno **wadudi** limetumiwa kama kisawe cha **latifu** katika ubeti wa 64. Neno hili lina maana kuwa sifa za Mungu ni nyingi ajabu. Aidha, mtunzi ametumia neno hili kusisitiza kuwa sifa za Mungu hazina idadi wala kipimo. Urudiaji huu umetumiwa na mtunzi kama njia ya kutambulisha na kusisitiza sifa za Mungu kama mhusika mkuu katika utenzi huu.

**Urudiaji wa Kiesajesia**

Urudiaji wa kiesajesia ni urudiaji wa kisemantiki unaohusu kurudiwa kwa wazo fulani kwa kutumia tamathali ya usemi. Mawazo mbalimbali yanarudiwa katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* kwa kutumia mbinu ya sitiari. Mfano ni katika ubeti wa 68 na 69. Katika beti hizi, mtunzi anasisitiza kuwa Mtume Muhammad ni mwangaza, nuru na tena tiba kwa matatizo yanayowakumba

Waislamu. Kwa hivyo, Waislamu wakifuata njia za Mtume, basi hawatapotea kamwe. Zaidi ya hayo, watapata suluhisho kwa matatizo yanayowakumba. Maneno "Mtume wetu ni taa" na "Mtume wetu ni dawa" yanatumiwa kuendeleza ujumbe kuwa Mtume Muhammad ndiye kiongozi na tena jibu kwa matatizo yote yanayowapata Mwislamu. Mbinu hii imechangia katika kuleta taswira au picha katika utungo huu. Hasa Mtume anapolinganishwa na taa. Yaani mwangaza ulio na mng'aro usio na kikomo.

Mifano zaidi ni katika beti hizi; ubeti wa 194, 231, 292, 403, 505, 531 na 536. Katika beti hizi Mudhari bin Darimi anamrejelea Sheikh Ali kama Simba wa Mungu. Kwa maana kuwa yeye ndiye mtetezi wa dini ya Kiislamu. Kulingana na msimulizi, hakuna mtu mwingine anayetetea na hata kupigania dini ya Kiislamu kwa njia sawa na Sheikh Ali. Isitoshe, mhusika huyu ameonyesha ujasiri wa hali ya juu anapoipigania dini.

**Urudiaji wa Usemi Maalum**

Kwa maoni yetu tunaweza kusema kuwa usemi maalum ama usemi ule ule umerudiwa katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* kama njia ya kusisitiza wazo au ujumbe unaowasilishwa na mtunzi. Kwa mfano, katika ubeti wa 774, usemi **La ilaha illa-Llahu** umerudiwa mara tatu na mtunzi. Usemi huu umerudiwa kama njia ya kusisitiza kuwa katika dini ya Kiislamu hakuna Mungu mwingine isipokuwa Allah. Aidha, katika dini hii, Allah ni mmoja tu na hakuna mwingine. Isitoshe, mtunzi anatusisitizia ya kwamba Muhammad ni Mtume na rasul wa mwisho wa Allah. Vilevile mtunzi anaeleza kuwa hakuna yeyote yule apasae kuabudiwa ila Mungu au Allah pekee.

Mtunzi anamsisitizia Mwislamu kuwa ni Allah pekee ndiye anastahili kuabudiwa bila mshirika. Kwa hivyo, kwa Mwislamu ni hatia kuabudu sanamu ama kiumbe kingine kile. Tunaweza kusema kuwa kifungu hiki kimerudiwa mara tatu kama njia ya kusisitiza ujumbe kuhusu dini ya Kiislamu. Ujumbe huu ni muhimu kwa Mwislamu kwa sababu ni nguzo au msingi wa dini. Mfano wa pili ni katika ubeti wa 775. Katika ubeti huu, mtunizi amerudia usemi "**Ya Allahu ya Kariimu**, **Ya Allahu tukirimu** na **Ya Allahu turahamu**." Katika mfano huu, mtunzi anasisitiza kuwa Mungu ni mkarimu na tena yeye ndiye mwenye kutoa msamaha na hata kuwakwamua waja kutoka kwa mambo ya dunia. Urudiaji huu wa usemi ule ule umetumiwa kama njia ya kuendeleza ujumbe kuhusu msamaha unaotolewa na Allah kwa Waislamu. Urudiaji wa usemi maalum wenye maana ile ile unatokea katika beti mbalimbali katika utenzi huu na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kukuza urudiaji wa kisemantiki.

**Urudiaji wa Mawazo Sawa**

Urudiaji wa wazo au mawazo sawa katika utungo huu ni aina ya urudiaji wa kisemantiki ambao unatokea wakati mtunzi anapozungumzia wazo fulani mwanzoni mwa kazi yake kisha suala hili linarudiwa tena baadaye kwa kutumia maneno yale yale ama kwa kutumia maneno tofauti lakini yanaleta maana ile ile kama ilivyokusudiwa hapo awali. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*, mtunzi amezungumzia suala la Siku ya Kiyama katika ubeti wa 21. Suala hili linahusu hukumu watakaopata waja siku ya mwisho. Mtunzi anasisitiza kuwa watu watahukumiwa siku hii kwa kutegemea kiwango chao cha dhambi.

Mtunzi anasimulia kuwa wale waliotenda mema wataruhusiwa kuenda Peponi kusherehekea huku watenda dhambi wakiteseka motoni kule Jehanamu. Isitoshe, mtunzi anawahimiza Waislamu kuwa watende kulingana na matakwa ya dini kwani hata majoka yatawauma watakaoenda Jehanamu. Aidha, anaelezea kuwa siku hii ya masiku itakuwa siku ya maangamio na mateso. Mawazo haya yamerudiwa na mtunzi katika ubeti wa 604- 653.

Usimulizi huu unatumiwa na mtunzi kama njia ya kusisitiza umuhimu wa kutubu na kufuata njia za kidini. Mtunzi anaendeleza dhamira ya toba na umuhimu wa kufuata dini ya Kiislamu kama njia ya kujiepusha na maangamio yatakayowapata waja Siku ya Kiyama. Mawazo sawa yamerudiwa katika beti mbalimbali katika utenzi huu na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kukuza urudiaji wa kisemantiki.

**Hitimisho**

Katika makala haya, tumeangazia urudiaji wa kisimulizi na wa kisemantiki kama mtindo unaofanikisha fani na maudhui katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*. Katika uhakiki huu, tumedhihirisha jinsi mtunzi wa utenzi huu alivyotumia aina mbalimbali za urudiaji wa kisimulizi na wa kisemantiki. Aidha, tumeonyesha vile urudiaji wa kisimulizi na wa kisemantiki unavyochangia katika kujenga fani na maudhui katika utungo huu. Kwa mfano, mtunzi anapotumia urudiaji wa semiki ambao ni aina ya urudiaji wa kisemantiki, sifa bainifu za wahusika mbalimbali zinaonyeshwa. Sifa hizi zinaandamana na matendo mbalimbali yanayokamilisha shughuli za utungo huu na kuleta dhamira. Sifa hizi pamoja na dhamira zimesheheni katika utungo huu na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kukuza urudiaji wa kisemantiki. Tunaweza kusema kuwa mhusika kama vile **Ibilisi** ana sifa; +uovu, -utakatifu, +giza.

Kwa upande wa pili mhusika kama vile **Mtume Muhammad** ana sifa kama vile; -uovu, +utakatifu, -giza. Hatimaye tumeonyesha vile urudiaji wa vitushi na wahusika unavyochangia maudhui na fani katika utenzi huu kwa ujumla. Tumebainisha kuwa mtunzi anaporudia hadithi, basi anafanya hivyo kama njia ya kusisitiza ujumbe wa hadithi hiyo. Isitoshe, wahusika wenye wanaongoza katika shughuli mbalimbali wanarudiwa kama msingi wa matendo na dhamira. Wahusika hawa ni kama vile; Allah, Mtume Muhammad, Isa, Ibilisi, Mudhari bin Darimi, malaika mbalimbali na Sheikh Ali. Wahusika hawa wametokea katika vitushi na beti mbalimbali na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kukuza urudiaji wa kisimulizi na kisemantiki.

**Marejeleo**

Aristotle, (1967). *Aristotle*: *Poetics*. Translated by Else, G. F). Ann Arbov: University of Mitchigan Press.

Leech, G. N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman Group.

Polkinghorne, D. E. (1995). *Narrative Configuration in Qualitative Analysis*. In International Journal of Qualitative Studies in Education. V8 P. G5-23.

Stanhope, N. & Cohen, G. & Conway, M. (1993). 'Very Long Term Retention of a Novel'. *Applied Cognitive Psychology*, 7:239-256.

Tsur, R. (2008). *Toward a Theory of Cognitive Poetics*. Sussex Academic Press, Brighton, 2nd Edition.

Wales, K. (2001). *A Dictionary of Stylistics*. London: Pearson Education.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi* l: *Msingi wa Uchanganuzi wa Kiswahili wa Fasihi*. Nairobi: Vide- Muwa Publishers Ltd.

Whelan, K. K., Huber, J., Rose, C., Davies, A. & Cladinin. J. (2010). 'Telling and Retelling Our Stories on the Professional Knowledge Landscape'. *Teachers and Teachings*: Theory and Practice, 7:143-156.